OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI KIDAMALI,
S.L.P. 2412,
IRINGA.

Kumb. Na. IR/KIDS/JI/ 2021 REHE: 10 Desemba, 2020

JINA: ……..

NAMBA YA MTIHANI: ……

SHULE ATOKAYO: ……

ANUANI: ……

WILAYA …….. MKOA ……..

FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Awali ya yote ninachukua fursa hii kukupongeza kwa kufaulu mtihani wako wa darasa la saba, kitendo ambacho kimekuwezesha kuchaguliwa kujiunga na shule ya sekondari KIDAMALI kidato cha kwanza mwaka 2021

Ni matumaini yangu BAHATI hii utaitumia vizuri ili uweze kupata maarifa ya hali ya juu yatakayo kuwezesha kufanikiwa katika masomo na shughuli nyingine muhimu kama vile uzalishaji mali, michezo n.k.

Aidha ni tegemeo langu kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule hii pamoja na masharti yote ya kujiunga kama yalivyoorodheshwa hapa chini.

Shule ipo Kata ya Nzihi katikati ya Kijiji cha NZIHI na KIDAMALI kandokando ya barabara iendayo Hifadhi ya Taifa ya Ruaha – Iringa, mita mia tatu (300) toka barabarani. Shule hii ni ya kutwa na ni mchanganyiko na ina Hosteli kwa watotowa kike.

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**lakini kidato cha kwanza anatakiwa kufika shule Tarehe **04/01/2021**pamoja na Mzazi/ Mlezi wake**BILA KUKOSA** ili aanze kusajiliwa mapema iwezekanavyo na apewe maelekezo muhimu ya shule hususani wajibu wake.

A) SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ikiwa safi wakati wote.

i. Akiwa masomoni darasani.
ii. Atakapokuwa anatoka nje ya shule.
iii. Kwenye Baraza la shule.
iv. Atakapokuwa anakwenda hospitali.
v. Kwenye maandamano.
vi. Atokapo nyumbani kwenda shuleni na anaporudi nyumbani.
vii. Sweta rangi ya JANI LA MGOMBA- kama huielewi fika shuleni uione

- Sketi na suruali ni za khaki, shati jeupe mikono mirefu.
- Sketi iwe ndefu, kugusa soksi na suruali siziwe**mlegezona zisiwe za kubana. sare zitashonwa na mafundi tuliowapa maelekezo tu.**
- **Sare unaweza kuzishona wakati ukiwa tayari shuleni- usichelewe kusubiri sare njoo na nguo za nyumbani.**

VIFAA VIFUATAVYO MZAZI UNATAKIWA UVINUNUE NA UVILETE SHULE

i. Viatu vya ngozi VYEUSI visivyo na kisigino kirefu.
ii. Soksi pea mbili au zaidi, wasichana NYEUPE wavulana VYEUSI.
iii. Raba kwa ajili ya michezo na bukta kwa wote, tracksuit nyeusi yenye mistari myeupe mitatu pembeni NA RABA NYEUPE.
iv. Kadi ya TIKA ama CHF au Bima ya Afya.
v. cheti cha kuzaliwa
vi. Ufagio mmoja wa chelewa.

B) VIFAA VYA KITAALUMA

i. Mathematical set (mkebe 1).
ii. Kalamu za wino nyeusi au bluu na kalamu ya risasi.
iii. Daftari 12 kubwa.(Counter book)
iv. Rula ndefu moja.
v. Mfuko wa kuhifadhia daftari, vitabu na vifaa vingine(School bag).

C) SHERIA ZA SHULE

i. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule wakati wa masomo bila idhini ya mwalimu wa darasa na zamu.
ii. Kuwaheshimu wafanyakazi wote waliopo hapa shuleni na watu wote wanaomzidi umri.
iii. Kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri, anapopita au kuingia mahali ulipo.
iv. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi, ugonjwa, kifo n.k.
v. Kuheshimu na kuthamini kazi za aina zote.
vi. Kutii mara moja unapoitwa.
vii. Kuheshimu bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, ofisi za shule na mali ya umma.
viii. Kuheshimu taratibu na kanuni zilizowekwa na shule.

ix. Kukaa kimya darasani, na kutoka kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyopo darasani.
x. Baadhi ya tabia ambazo haziruhusiwi kwa mwanafunzi ni:-
    - Kutembelea maeneo ya vilabu vya pombe, nyumba za wageni.
    - Kuvuta sigara, bangi, kutumia madawa ya kulevya, kunywa pombe n.k.
    - Kucheza kamali.
    - Kufuga nywele, ndevu, na kuvaa mavazi yasiyo na heshima.
    - Kugombana, kupigana, kutukanana n.k.
    - Uasherati, wizi, utapeli n.k.

D) MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE NI

i. Wizi.
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga.
iii. Uvutaji bangi na ulevi wa aina yeyote.
iv. Kuoa au kuolewa.
v. Makosa ya jinai.
vi. Kupigana au kupiga.
vii. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
viii. Kutoa mimba.
ix. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
x. Utoro wa shule.
xi. Utovu wa nidhamu kwa ujumla.
xii. Kukataa adhabu, kuchochea na kuongeza au kuvuruga amani na usalama wa watu.

F) WAGONJWA

Wagonjwa wote watapata kibali cha kwenda hospitali kupitia mwalimu wa zamu.

G) UTORO

Mwanafunzi ambaye hatahudhuria shuleni bila taarifa atahesabiwa kuwa ni mtoro. Taarifa kuhusu mwanafunzi asiyehudhuria shuleni kutokana na matatizo yeyote lazima taarifa ziwasilishwe shuleni siku hiyo ya matatizo kwa mwalimu wa zamu au walimu wa malezi na mzazi/ mlezi anayetambuliwa na shule kulingana na fomu za usajiri

Ni matumaini yangu kuwa utazingatia maelezo hayo.

_____

YORAM L. MPONZI

MKUU WA SHULE

0769690315/0712449258

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KIDAMALI,
S.L.P. 2412,
IRINGA.

A: MWANAFUNZI

Mimi …….. nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na shule, ninakubali/ sikubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Kidamali. Na ninaahidi kuwa nitazingatia kanuni na sheria zote za shule. Nitafuata masharti yote yatakayotolewa na Mkuu wa shule, wafanyakazi na viongozi wote shuleni. Ninaahidi pia kuwa nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, kazi za nje na katika michezo kwa muda wote.

Dini yangu …… (Mkristo, Mwislamu n.k) hutaruhusiwa kubadili dini ukiwa hapa shuleni bila idhini ya mzazi/ mlezi.

Sahihi …… Tarehe …….

B: MZAZI/ MLEZI

Mimi …….. mlezi/ mzazi wa …….. ambaye amechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Kidamali. Nimesoma kwa makini maagizo ya kujiunga na shule na sheria zake, ninakubali/ nikatakaa nafasi hiyo. Ninaahidi kumtimizia mtoto wangu maagizo yote ya kujiunga na shule hii katika muda uliopangwa.
Pia nitashirikiana daima na shule katika kumkuza na kumlea mtoto wangu.

Ahsante.

Jina la Mzazi/ Mlezi: ……
Anuani S.L.P.: ……
Kijiji cha: ……
Kitongoji cha ……

Tarehe …….. Sahihi …….

Futa isiyostahili
Mzazi/ mlezi ukibadilisha anwani tujulishe anwani mpya mara moja.

(KITAMBULISHO B)

KIDAMALI SECONDARY SCHOOL,
P.O. Box 2412,
IRINGA.

Date: ……

MEDICAL OFFICER,
GOVERNMENT HOSPITAL,
……..
……

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Name of student ……

Please, examine the above named to his/ her fitters as indicated below. Please arrange for necessary treatment so that the certificate may be assigned and brought to school by student.

The certificate must be signed by a qualified medical officer of Government Hospital.

Date …….. Signature …….

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named student with:-

Skin …….	Abdomen …….
Eyes …….	Stool …….
Ear ……	Urine …….
Teeth …….	H/B (Hemoglobin) …….
VD …….	TB Test …….

Any other disabilities ……

1. Consider that ……. (name of student) is in good health free from infection disease, worms and fit to come to school.
2. He/ she is fit to come to school after having treatment of …….
3. She is/ not pregnant ……..
4. Other comments (if any) ……

……

…… ……

SIGNATURE **DESIGNATION**

Date: ……..

PUPILS

NB: You must bring this complete form when you come to school, no pupils may be enrolled without certificate of physical fitness.